TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

PONGEZI KWA SERIKALI YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KWA KUMUHAKIKISHIA **MTOTO WA KIKE HAKI YA ELIMU**

Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) na wadau wake tuna furaha kuipongeza Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya uongozi wa Mh. Raisi Samia Suluhu Hassan, kufuatia tamko lililotolewa Novemba 24, 2021 na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ambapo Mhe. Profesa Joyce Ndalichako alieleza rasmi kwamba wanafunzi wa shule za msingi na sekondari waliokatishwa masomo kwa sababu mbalimbali ikiwemo utoro, mimba, na changamoto mbalimbali za kifamilia watapewa fursa ya kurejea shuleni katika mfumo ulio rasmi.

Kufikia mwaka 2020 idadi ya wasichana 6,475 hukatishwa masomo kila mwaka kutokana na mimba za utotoni, ambapo 1,135 hutoka shuke ya msingi na 5,340 kutoka Sekondari. Hii inaonesha ni kwa kiasi gani mimba za utotoni zimekuwa kikwazo kwa wasichana wengi katika kufikia ndoto zao za kielimu, na kuchangia kuwepo kwa pengo la jjinsia kati ya wasichana na wavulana wanaomaliza elimu ya sekondari. Hatua hii ya serikali ya kutoa fursa kwa wasichana waliokatishwa masomo kurejea shuleni inawapa nafasi ya kunufaika na mfumo rasmi wa kielimu ambao huwaendeleza kitaaluma pamoja na kuwapatia ujuzi kwa ajili ya maendeleo ya mtu binafsi na ujuzi wa kujitegemea ikiwemo masuala ya uongozi, afya ya uzazi.

TGNP na wadau wake, tumefurahishwa na kauli hii kwani inaonesha nia ya dhati ya Serikali katika kuleta usawa wa kijinsia katika upatikanaji wa elimu. Hatua hii pia inaonesha nia ya dhati ya serikali ya kutekeleza

dira ya Taifa 2025 na makubaliano mbalimbali ya kikanda na kimataifa ambayo nchi imeridhia ikiwemo Makubaliano ya Haki za Binadamu (Makubaliano ya Maputo) 2003, Makubaliano ya Jinsia na Maendeleo kwa Nchi za SADC 2008, Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Mtoto ya 1989, Malengo ya Maendeleo Endelevu (2015) hususan lengo namba nne (4) na tano (5), na makubaliano mengine kama Mapatano ya Kimataifa ya Kutokomeza Aina zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake 1979, na mengineyo.

Tunatoa rai kwa wadau wa maendeleo na AZAKI kuunga mkono na kufanya kazi pamoja na Serikali katika kuhakikisha maazimio na maagizo ya serikali katika kutekeleza tamko hili la kuwarudisha shule wanafunzi waliopata ujauzito na changamoto nyingine. Ni jukumu letu kuendelea kuisaidia serikali kuielimisha jamii kuondoa mitazamo hasi juu ya mabinti waliojifungua na kurudi shule. Upo uhitaji mkubwa wa kutoa unasihi kwa mabinti, familia, jamii, wanafunzi wenzao pamoja na walimu, ili waweze kulipokea suala hili kwa namna chanya na kutoa msaada stahiki kwa mabinti hawa.

Tunashauri Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia kuhakikisha kuwa tamko hili linakuwa sheria ambapo kila mwanafunzi wa kike aliyekumbana na changamoto hii atakuwa na haki ya kurejea shuleni. Sambamba na hilo, Serikali inapaswa kuboresha sheria, mifumo na mikakati mbalimbali ili kuwapa watoto kike ulinzi dhidi ya ukatili wa kijinsia ambao unapelekea kukwamisha ndoto zao. Vile vile, tunatoa wito kwa serikali kutenga bajeti ya kutosha ili kuwezesha utekelezaji stahiki wa afua za kukomesha ukatili wa kijinsia kupitia Mpangokazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA).

Katika hatua za uboreshaji wa ulinzi wa Watoto wa kike, tunapendekeza yafuatayo:

1. Serikali kutilia mkazo utekelezaji wa sheria adhabu ya makosa ya jinai namba 16 inayolinda haki za wanawake na watoto wa kike, kwa kuhakikisha kifungo cha miaka 30 kwa yeyote atakayempa mimba mtoto wa kike. Hii itasaidia kutokomeza kabisa mimba za utotoni.

2. Kuweka mfumo unaotunza kumbukumbu za watoto wa kike wanaoacha shule na kuwafuatilia pindi wanapojifungua kuanzia ngazi ya vijiji na mitaa ili kuhakikisha wanatambuliwa na kupewa fursa na haki yao ya msingi ya kupata elimu.
3. Kuboresha ushirikiano kati ya walimu na wazazi ili kuwezesha wazazi wenye uwezo wa kutoa unasishi na elimu ya malezi na makuzi kushiriki kuwapa eliimu na kuongea na watoto wa kike, ikiwemo kuwaeleza juu ya kujilinda. Hii iende sambamba na kuhakikisha kuwa kila shule ina walimu wa kike.
4. Katika marekebisho ya mitaala yanayoendelea, Wizara ya Elimu Irejeshe elimu ya kujitegemea kuanzia mitaala ya shule za msingi ili kuwapa watoto fikra sahihi ya kupenda kujitegemea na kuepuka vishawishi.
5. Wizara ya Afya kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa afya na maendeleo inatakiwa kuweka nguvu ili watoto waweze kuelimishwa mapema kuanzia wakiwa wadogo juu ya elimu ya afya ya uzazi ili waweze kutambua mabadiliko yanayotokea kwenye miili yao na kufanya maamuzi sahihi.

Aidha, tunatoa wito kwa Serikali na wadau wengine kutafuta mzizi au chanzo cha tatizo hili la mimba za utotoni na kutafuta utatuzi wake ili kuwanusuru mabinti kubeba jukumu hili la uzazi ambalo halilingani na umri wao.

TGNP na wadau wake tunaahidi kuendelea kutoa ushirikiano kwa Serikali katika nyanja mbali mbali ili kuweza kufanikisha lengo la kuleta usawa wa jinsia na kuwezesha wanawake na watoto wa kike nchini.

Tamko limetolewa na:
Lilian Liundi

Mkurugenzi Mtendaji
Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP)



TGNP

P.O Box 8921, Dar es Salaam, Tanzania

Ubungo Industrial Areas | Mabibo Road

Tel: +255 754 784 050

Email: info@tgnp.or.tz

Website: www.tgnp.or.tz

@tgnptz @tgnptz @tgnptz1